# SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI KUHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA SERIKALI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**MASHARTI YA AWALI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

**SEHEMU YA PILI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA KODI NAM. 7 YA 2009**

2. Kusomwa.
3. Marekebisho ya kifungu cha 3.
4. Marekebisho ya kifungu cha 4.
5. Marekebisho ya kifungu cha 7.
6. Marekebisho ya kifungu cha 21.
7. Marekebisho ya kifungu cha 22.
8. Kuongeza kifungu kipya cha 22A.
9. Marekebisho ya kifungu cha 23.
10. Marekebisho ya kifungu cha 24.
11. Marekebisho ya kifungu cha 31A.
12. Marekebisho ya kifungu cha 43.

13. Marekebisho ya kifungu cha 51.

14. Kuongeza kifungu kipya cha 52A.

15. Kuongeza kifungu kipya cha 53B.

**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI NAM. 4 YA 1998**

16. Kusomwa.

17. Marekebisho ya kifungu cha 2.

18. Marekebisho ya kifungu cha 5.

19. Marekebisho ya kifungu cha 6.

20. Marekebisho ya kifungu cha 16.

**SEHEMU YA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI ZA MAFUTA NAM. 7 YA 2001**

21. Kusomwa.

22. Marekebisho ya kifungu cha 2.

23. Marekebisho ya kifungu cha 3.

**SEHEMU YA TANO**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAENDELEO YA KARAFUU NAM. 2 YA 2014**

24. Kusomwa.

25. Marekebisho ya kifungu cha 3.

26. Marekebisho ya kifungu cha 19.

27. Kuongeza vifungu vipya vya 19A, 19B na 19C.

28. Kuongeza vifungu vipya vya 26A na 26B.

29. Marekebisho ya kifungu cha 27.

30. Marekebisho ya kifungu cha 29.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA AJIRA NAM. 11 YA 2005

31. Kusomwa.

32. Marekebisho ya kifungu cha 100.

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAFUNZO YA AMALI NAM. 8 YA 2006

33. Kusomwa.

34. Marekebisho ya kifungu cha 27.

SHERIA NAMBA 6 YA 2017

NIMESAINI

{DR. ALI MOHAMED SHEIN}
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

30 Juni ..............................................., 2017

# SHERIA YA KUTOZA KODI NA KUREKEBISHA BAADHI YA SHERIA ZA FEDHA NA KODI KUHUSIANA NA UKUSANYAJI NA UDHIBITI WA MAPATO YA SERIKALI NA MAMBO MENGINE YANAYOHUSIANA NA HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## MASHARTI YA AWALI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Fedha (Usimamizi wa Fedha za Umma) 2017 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA USIMAMIZI WA KODI NAM. 7 YA 2009

Kusomwa.

**2.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Usimamizi wa Kodi Nam. 7 ya mwaka 2009 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**3.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri mpya ya maneno kulingana na mpangilio wa alfabeti kama ifuatavyo:

> "Mashine za kielektroniki" maana yake ni mashine maalum zinazotumika katika biashara, kwa kutambua upokeaji, uchambuzi wa mauzo na mfumo wa udhibiti wa bidhaa; na inajumuisha mfumo wa kompyuta wa kutolea stakabadhi, mfumo wa usajili wa stakabadhi, mashine za kutolea stakabadhi katika pampu za mafuta na simu za mkononi"

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**4.** Kifungu cha 4(5) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "kanuni maalum za biashara" yanayojitokeza baada ya neno "pamoja" na kuweka badala yake maneno "thamani ya soko huru".

Marekebisho ya kifungu cha 7.

**5.** Kifungu cha 7 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuingiza kifungu kidogo kipya cha (7) mara baada ya kifungu kidogo cha (6) kama ifuatavyo:

**"(7).** Kamishna atakuwa na uwezo wa kuhamisha usajili wa mlipakodi kutoka aina moja ya kodi kwenda nyengine ikiwa mlipakodi huyo atashindwa kutimiza masharti ya usajili kwa aina ya kodi aliyosajiliwa awali."

(b) kwa kukipa nambari mpya kifungu kidogo cha (7) kuwa kifungu kidogo cha (8).

Marekebisho ya kifungu cha 21.

**6.** Kifungu cha 21 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "ya rufaa" yanayojitokeza baina ya neno "haki" na neno "chini ya" na kuweka badala yake maneno " kuweka pingamizi".

Marekebisho ya kifungu cha 22.

**7.** Kifungu cha 22(1) cha Sheria Mama kinarekebishwa katika:

(a) aya (a), kwa kufuta maneno " stakabadhi ya mauzo taslimu" na maneno" ankara ya kodi" na kuweka badala yake maneno "stakabadhi ya malipo ya kielektroniki" na "ankara ya kodi ya kielektroniki" katika mpangilio wake.

(b) aya (b), kwa kuingiza neno "kieletroniki" baina ya maneno "yote" na "kodi" na baina ya maneno "na" na "stakabadhi".

Kuongeza kifungu kipya cha 22A.

**8.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza, mara baada ya kifungu cha 22, kifungu kipya cha 22A kama ifuatavyo:

" Mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kupokea na kutuma nyaraka.

22A.-(1) Kamishna anaweza kuanzisha na kuendesha mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kupokea, kutunza na kutuma nyaraka.

(2)Waziri atatunga kanuni zitakazosimamia mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kupokea, kutunza na kutuma nyaraka.

Marekebisho ya kifungu cha 23.

**9.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 23 na kuweka badala yake kifungu kipya kama ifuatavyo:

"Matumizi ya malipo ya kielektroniki.

23.-(1) Mtu ambaye anauza bidhaa au anatoa huduma iwe kwa mkopo au kwa malipo au anaepokea malipo kwa bidhaa zilizouzwa au huduma zilizotolewa atalazimika kutoa stakabadhi ya malipo ya kielektroniki au ankara ya kielektroniki kwa kutumia mashine ya kielektroniki.

(2) Bila ya kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Kamishna anaweza kumsamehe mtu au kikundi cha watu kutoa

stakabadhi ya malipo ya kielektroniki au ankara za kielektroniki kwa kutumia mashine ya kielektroniki.

(3) Kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha (2), Kamishna atatangaza katika gazeti linalosomwa zaidi au katika chombo chochote cha habari cha umma, orodha ya majina ya watu au makundi ya watu waliosamehewa kutokana na matakwa ya kutoa stakabadhi za malipo au ankara kwa kutumia mashine ya kielektroniki.

(4) Mtu ambaye amesamehewa kutumia mashine ya kielektroniki atatoa stakabadhi ya kawaida ya malipo, mauzo au ankara ya kodi.

(5) Mtu anayetoa stakabadhi ya kawaida ya malipo ataingiza au atawezesha kuingizwa katika stakabadhi ya mauzo au ankara ya kodi na kivuli cha nakala za taarifa zilizoainishwa katika kanuni.

(6) Stakabadhi ya kawaida ya malipo, mauzo au ankara ya kodi zitachapishwa kwa mtiririko wa nambari na kwamba hakuna nambari itakayotolewa zaidi ya mara moja.

(7) Mtu yeyote anayekwenda kinyume na masharti ya kifungu hiki atakuwa anatenda kosa na atakapotiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua Shilingi Laki Moja au asilimia kumi (10%) ya kodi inayopaswa kulipwa, yoyote itakayokuwa kubwa."

Marekebisho ya kifungu cha 24.

**10.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 24 na kuweka badala yake kama ifuatavyo:.

"Kodi inayooneshwa kuhusiana na ankara ya kodi, stakabadhi ya malipo au mauzo.

**24.** Kiwango chochote kinachooneshwa katika ankara ya kodi ya kielektroniki, stakabadhi ya malipo ya kielektroniki au stakabadhi ya mauzo au hati nyengine yoyote kama ni kiwango cha kodi kilichotozwa kuhusiana na mauzo ya bidhaa au huduma, kitawajibika kulipwa kama deni la kodi kutoka kwa mtu aliyetoa hati hiyo bila ya kujali kwamba:

(a) ankara ya kodi ya kieletroniki, stakabadhi ya malipo au stakabadhi ya mauzo au hati nyengine yoyote ipo katika mfumo ulioelezwa katika Sheria;

(b) kodi imeshatozwa kuhusiana na mauzo ambayo hati hiyo inahusika;

(c) mtu anayetoa ankara ya kodi ya kieletroniki, stakabadhi ya malipo ya kielektroniki au mauzo au hati nyengine yoyote ni mlipakodi.

Marekebisho ya kifungu 31A.

**11.** Sheria Mama inarekebishwa katika kifungu cha 31A kwa:

(a) kukipa nambari kifungu cha 31A kuwa kifungu cha 31A (1);

(b) kufuta aya (a) na kuweka badala yake kama ifutavyo:

"(a) ankara ya kodi ya kieletroniki, stakabadhi ya malipo au stakabadhi ya mauzo imetolewa";

(c) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Kamishna anaweza kuruhusu malipo ya kodi kwa mfumo wa malipo wa simu za mkononi, malipo ya kielektroniki au njia nyengine yoyote itakayoelezwa na Kamishna.

(d) kuongeza kifungu kidogo kipya cha (3) kama ifuatavyo:

"(3) Iwapo mlipakodi atafanya malipo ya kodi kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1), atamjuilisha Kamishna kuhusu malipo hayo".

Marekebisho ya kifungu cha 43.

**12.** Kifungu cha 43 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (1) kwa kuongeza aya mpya za (e) na (f) mara tu baada ya aya (d) kama ifuatavyo:

"(e) ikiwa mlipakodi atajaribu kumzuia Kamishna au Ofisa aliyeidhinishwa katika kutekeleza majukumu au wajibu wake chini ya Sheria hii;"

"(f) ikiwa mlipakodi amepewa taarifa ya kutenda kosa kwa mujibu wa kifungu cha 52A na akashindwa kufika mbele ya Kamishna katika tarehe iliyoelezwa katika taarifa hiyo".

Marekebisho ya kifungu cha 51.

**13.** Kifungu cha 51 (1) na (2) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa:

(a) kuingiza neno "kielektroniki" baina ya maneno "malipo"na "stakabadhi" na baina ya maneno "au" na "kodi" katika kifungu kidogo cha (1);

(b) kuingiza neno "kielektroniki" baina ya maneno "malipo" na "stakabadhi" na baina ya maneno "au" na "kodi" katika kifungu kidogo cha (2).

Kuongeza kifungu kipya cha 52A.

**14.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 52A mara baada ya kifungu cha 52 kama ifuatavyo:

“Notisi ya kutenda kosa.

52A.-(1) Pale ambapo Kamishna atakuwa na sababu za kuamini kuwa mtu ametenda kosa chini ya Sheria hii au sheria nyengine yoyote ya kodi, atatoa notisi ya kutenda kosa kwa mtu huyo.

(2) Notisi ya kutenda kosa itajumuisha mambo yafuatayo:

(a) jina na anuani ya mkosa;

(b) nambari ya Utambulisho ya Mlipakodi;

(c) nambari ya Usajili;

(d) maelezo ya kosa lililotendwa;

(e) tarehe na mahala ambapo mlipakodi atatakiwa kufika mbele ya Kamishna;

(f) saini ya ofisa aliyetoa notisi ya kutenda kosa; na

(g) taarifa nyengine yoyote ambayo Kamishna ataona inafaa.

(3) Mtu yeyote ambaye notisi imetolewa kwake na akashindwa kufika mbele ya Kamishna kwa tarehe na mahali palipoainishwa katika notisi, atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atapaswa kulipa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano au adhabu ya kifungo kisichopungua mwaka mmoja.

Kuongeza kifungu kipya cha 53B.

**15.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza kifungu kipya cha 53B mara baada ya kifungu cha 53A kama ifuatavyo:

“mifumo ya kupata faida ya kodi isiyokubalika.

53B.-(1) Bila ya kujali masharti yoyote ya Sheria hii, Kamishna anaweza kuamua wajibu wa kulipa kodi yoyote na kiwango chake, kama kwamba mifumo haijaingiliwa au kutekelezwa au kwa namna yoyote itakavyojitokeza kukinga au kupunguza faida ya kodi inayopatikana kutokana na mfumo huo.

(2) Maamuzi chini ya kifungu kidogo cha (1) yatachukuliwa kuwa ni tathmini ya kodi, na masharti ya Sheria hii yanayohusiana na tathmini ya kodi yatatumika ipasavyo.

(3) Katika kifungu hiki “malengo mazuri ya kibiashara” haijumuishi kupata faida ya kodi na “faida ya kodi” inajumuisha:

(a) ukwepaji kodi au kupunguza wajibu wa mtu yoyote wa kulipa kodi;

(b) ongezeko lolote kwa mlipakodi katika marejesho ya kodi;

(c) punguzo lolote katika makubaliano lililolipwa na mtu yeyote kuhusiana na mauzo ya bidhaa au huduma au uingizaji wa bidhaa yoyote; au

(d) ukwepaji kodi mwengine wowote au kuakhirisha wajibu wa kulipa kodi yoyote.

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI NAM. 4 YA 1998

Kusomwa.

**16.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Nam. 4 ya 1998 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**17.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri mpya ya maneno kulingana na mpangilio wa alfabeti kama ifuatavyo:

"Huduma za kifedha" maana yake ni:

(a) utoaji, kufanya makubaliano na kujihusisha na utoaji wa mikopo, dhamana ya mikopo na amana ya kifedha ikijumuisha usimamizi wa mikopo au dhamana ya mikopo kwa mdhamini;

(b) miamala inayohusiana na uwekaji wa fedha, akaunti ya hundi ya malipo, uhaulishaji, madeni, hundi, au miamala inayoweza kubadilishwa kwa fedha ambao si ukusanyaji wa madeni au ulipaji wa madeni;

(c) miamala inayohusiana na huduma za kifedha za malipo ya baadae, mikataba ya malipo ya baadae, njia za kupata hati ya kifedha na taratibu nyengine zinazofanana na hayo;

(d) miamala inayohusiana na hisa, sehemu ya hisa, dhamana na amana nyengine lakini haijumuishi huduma za utunzaji;

(e) miamala inayohusisha utoaji au uhaulishaji wa umiliki wa maslahi katika mfumo ambao unafanywa kwa malipo au utoaji wa mafao na mifuko ya mafao, mfuko wa mafao ya uzeeni, mfuko wa pensheni, mfuko wa malipo ya kustaafu kwa mwaka, mfuko wa hifadhi au mfuko unaofanana nayo;

(f) miamala inayohusisha utoaji au uhaulishaji wa umiliki wa mikataba ya bima au utoaji upya wa bima inayohusiana na mikataba hiyo;

(g) kufanya malipo au ukusanyaji kiwango cha faida, mtaji, gawio au kiwango chengine kinachohusiana na hisa, deni, amana ya mikopo, dhamana ya kawaida, dhamana ya ushiriki, mkataba wa mikopo, mkataba wa bima ya maisha au mkataba **wa** malipo ya baadae; na

(h) miamala ya ubadilishaji wa fedha ikijumuisha hundi za nje na hawala za kimataifa za fedha, lakini haijumuishi huduma za kupanga au kuwezesha huduma zilizoelezwa katika aya ya (a) hadi aya ya (g).

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**18.** Kifungu cha 5 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (7) mara baada ya kifungu kidogo cha (6) kama ifuatavyo:

"(7) Waziri anaweza kutunga kanuni kwa ajili ya ukusanyaji na hesabu ya Kodi ya Ongezeko la Thamani katika utoaji wa huduma za kifedha".

Marekebisho ya kifungu cha 6.

**19.** Kifungu cha 6 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) katika kifungu kidogo cha (2), kwa kuingiza neno" kieletroniki" baina ya herufi "a" na maneno "ankara ya kodi";

(b) katika kifungu kidogo cha (3) kwa kuingiza neno "kieletroniki" baina ya herufi "a" na maneno "ankara ya kodi".

Marekebisho ya kifungu cha 16.

**20.** Kifungu cha 16(4)(a) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza neno "kieletroniki" baina ya herufi "a" na maneno "ankara ya kodi".

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI ZA MAFUTA NAM. 7 YA 2001

Kusomwa.

**21.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi za Mafuta Nam. 7 ya 2001 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**22.** Kifungu cha 2 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri mpya ya maneno kulingana na mpangilio wa alfabeti kama ifuatavyo:

"mafuta yaliyosafishwa" maana yake ni aina za mafuta zilizoelezwa katika Jadweli la Kwanza la Sheria hii ambayo yanatokana na mafuta ghafi yaliyosafishwa Zanzibar".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**23.** Kifungu cha 3(1) cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingizwa maneno "na mafuta yaliyosafishwa" baina ya maneno "Zanzibar" na "kwa viwango":

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAENDELEO YA KARAFUU NAM. 2 YA 2014

Kusomwa.

**24.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Maendeleo ya Karafuu Nam. 2 ya 2014, katika Sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**25.** Kifungu cha 3 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri za maneno kulingana na mpangilio wa alfabeti kama ifuatavyo:

"taasisi" inajumuisha shirika linalojitegemea, jumuiya, chama cha ushirika, ubia, au taasisi nyengine inayolingana nayo;

"magendo" maana yake ni usafirishaji au uchukuaji usio halali katika chombo cha baharini, angani au nchi kavu, au uhaulishaji au uondoshaji usio halali wa miche ya mikarafuu, karafuu, makonyo ya karafuu au bidhaa zinazotokana na karafuu kwa madhumuni ya kuzitoa sehemu moja kwenda sehemu nyengine ndani au nje ya Zanzibar".

Marekebisho ya kifungu cha 19.

**26.** Kifungu cha 19 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) katika kifungu kidogo cha (1), kwa kuingiza neno "au" baina ya maneno "karafuu" na "makonyo";

(b) kwa kufuta kifungu kidogo cha (5) na cha (6) na badala yake kuweka vifungu vidogo vipya vya (5) na (6) kama ifuatavyo:

"(5) Mtu anayekiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) au kifungu kidogo cha (4) cha kifungu hiki atakuwa ametenda kosa".

"(6) Waziri anaweza kuweka utaratibu wa utekelezaji mzuri wa kifungu hiki."

Kuongeza vifungu vipya vya 19A, 19B na 19C.

**27.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 19, vifungu vipya vifuatavyo:

" Kupiga marufuku magendo ya karafuu.

19A.- (1)Ni kosa kwa mtu yeyote kufanya lolote kati ya matendo yafuatayo:

(a) kufanya magendo ya karafuu, miche ya mikarafuu, makonyo ya karafuu na bidhaa zinazotokana na karafuu au kuzitoa sehemu moja kwenda sehemu nyengine ndani au nje ya Zanzibar;

(b) kujaribu kufanya magendo ya karafuu, miche ya mikarafuu, makonyo ya karafuu na bidhaa zinazotokana na karafuu kuzitoa sehemu moja kwenda sehemu nyengine ndani au nje ya Zanzibar;

(c) kula njama ya kufanya magendo ya karafuu, miche ya mikarafuu, makonyo ya karafuu na bidhaa zinazotokana na karafuu kuzitoa sehemu moja kwenda sehemu nyengine ndani au nje ya Zanzibar;

(d) kushiriki katika shughuli yoyote inayohusiana na kufanya magendo ya karafuu, miche ya mikarafuu, makonyo ya karafuu na bidhaa zinazotokana na karafuu kuzitoa sehemu moja kwenda sehemu nyengine ndani au nje ya Zanzibar.

(2) Mtu yeyote anayefanya lolote kati ya mambo yaliyokatazwa chini ya kifungu kidogo cha (1) atakuwa ametenda kosa, na akitiwa hatiani ataadhibiwa kama ifuatavyo:

(a) ikiwa mtu atatiwa hatiani chini ya kifungu kidogo cha (1) (a) cha kifungu hiki, atapewa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka saba na kisichozidi miaka kumi na tano na wakati anatumikia adhabu yake atapanda miche sabini elfu ya karafuu;

(b) ikiwa mtu atatiwa hatiani chini ya kifungu kidogo cha (1) (b), (c) au (d) cha kifungu hiki, atapewa adhabu ya kifungo kisichopungua miaka mitano na kisichozidi miaka kumi, na wakati anatumikia adhabu yake, atapanda miche ya mikarafuu elfu hamsini.

"Amri ya kutaifisha.

19B. Endapo mtu atatiwa hatiani kwa kosa la magendo chini ya Sheria hii, Mahakama, pamoja na adhabu ya kifungo, itatoa amri ya kutaifisha karafuu, miche ya mikarafuu, makonyo ya karafuu na bidhaa nyengine zinazotokana na karafuu, chombo cha usafiri wa nchi kavu, chombo cha usafiri wa bahari, chombo cha usafiri wa anga au chombo chochote kilichotumika wakati wa kutenda kosa.

"Kupiga marufuku ya uingizaji wa karafuu.

19C.- (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuingiza karafuu Zanzibar kwa madhumuni ya biashara.

(2) Mtu yeyote ambaye anakiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, atakuwa anatenda kosa na akitiwa hatiani, karafuu zilizoingizwa zitataifishwa.

(3) Endapo mtu atatiwa hatiani kwa kosa chini ya kifungu hiki, Mahakama, pamoja na adhabu iliyotolewa, itatoa amri kwa mtu huyo kulipa Serikalini kiasi cha fedha sawa na kilichopatikana kutokana na mauzo ya karafuu zilizotaifishwa.

Kuongeza vifungu vipya vya 26A na 26B.

**28.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kuongeza mara baada ya kifungu cha 26, vifungu vipya vifuatavyo:

"Kutoa siri za kuzuia magendo.

26A. Mtu ambaye anatoa siri zinazohusiana na operesheni za kuzuia magendo kwa mfanya magendo au kwa mtu mwengine yeyote ambaye hahusiki na operesheni atakuwa ni mkosa, na akitiwa hatiani, atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Tano au kifungo kisichopungua miaka mitano au adhabu zote mbili."

"Kutoa taarifa za uongo.

26B. Endapo mtu anahusika na operesheni ya kuzuia magendo au ana dhamana ya utekelezaji wa sheria, anatoa taarifa za uongo kwa mamlaka husika kwa madhumuni ya kudanganya, atakuwa ni mkosa na akitiwa hatiani atatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Saba au kifungo kisichopungua miaka saba au adhabu zote mbili."

Marekebisho ya kifungu cha 27.

**29.** Sheria Mama inarekebishwa kwa kufuta kifungu cha 27 na kuweka badala yake kifungu kipya kama ifuatavyo:

"Makosa yanayofanywa na taasisi.

27. Iwapo kosa lolote chini ya Sheria hii au chini ya kanuni zilizotungwa chini ya Sheria hii limefanywa na taasisi:

(a) mtu ambaye, wakati kosa linafanyika ni mkurugenzi au ni afisa mwenye dhamana ya mambo ya taasisi husika, atakuwa ni mkosa, na akitiwa hatiani ataadhibiwa ipasavyo; na

(b) taasisi itakuwa imetenda kosa na ikitiwa hatiani itatozwa faini isiyopungua Shilingi Milioni Kumi.

Marekebisho ya kifungu cha 29.

**30.** Kifungu cha 29 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuondoa neno "Mfuko" popote litakapojitokeza katika kifungu hiki na kuweka badala yake neno "Shirika."

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA AJIRA NAM. 11 YA 2005

Kusomwa.

**31.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Ajira Nam. 11 ya 2005 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 100.

**32.** Kifungu cha 100 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka badala yake kifungu kidogo cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Malipo ya mshahara yatafanywa kwa kuingizwa moja kwa moja katika hesabu ya muajiriwa katika benki iliyoteuliwa na muajiriwa."

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAFUNZO YA AMALI NAM. 8 YA 2006

Kusomwa.

**33.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mafunzo ya Amali Nam. 8 ya 2006 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama "Sheria Mama".

Marekebisho ya kifungu cha 27.

**34.** Kifungu cha 27 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (4) na kuweka badala yake kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

"(4) "Kwa madhumuni ya kifungu hiki malipo ya mshahara wa mwezi kuhusiana na muajiriwa yeyote inajumuisha mshahara halisi, maposho, kamisheni, bonasi na kiwango chochote kinacholipwa kuhusiana na ajira au huduma iliyotolewa na muajiriwa katika mwezi, isipokuwa haitajumuisha gharama za mafunzo na gharama za sare."

**UMEPITISHWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, tarehe 20 Juni, 2017.

..............................................................

(RAYA ISSA MSELLEM)
***Katibu wa Baraza la Wawakilishi***
***Zanzibar***